# TURNING VIEW 2021

## KISWAHILI : LUGHA

**002** **8**

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. *Tumia penseli ya kawaida tu.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-*

***(i)JINA LAKO*** ***(ii)JINA LA SHULE YAKO***

***Muda: Saa 1 Dak. 40***

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15 . Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Kusema si kazi, kazi ni ___1___ na ___2___ hivyo ___3___ ilivyokuwa kwa panya waliokutana ili ___4___ tatizo ___5___ paka kuwamaliza. Mashauri mazuri yaliyo ___6___ yalitolewa na wale panya ___7___. Lakini hakuna aliyekuwa tayari ___8___ kengele paka kwani huko ___9___ kujiangamiza ___10___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. kufanyiza | B. kufanyiwa | C. kutenda | D. kutendea |
| **2.** | A. vivyo | B. ndivyo | C. hivyo | D. ilivyo |
| **3.** | A. ndio | B. ndivyo | C. ndiwo | D. ndiko |
| **4.** | A. kutatia | B. kutatua | C. kutatiza | D. kutatisha |
| **5.** | A. ya | B. wa | C. za | D. la |
| **6.** | A. masafi | B. safika | C. safi | D. maswafi |
| **7.** | A. mahodari | B. hodari | C. walio hodari | D. vihodari |
| **8.** | A. kumfunga | B. kumfungia | C. kumfungulia | D. kumfungua |
| **9.** | A. ndimo | B. ndiko | D. ndilo | D. ndipo |
| **10.** | A. lenyewe | B. wenyewe | C. mwenyewe | D. chenyewe |

Niliandamana na wazazi wangu guu ___11___ guu pili ___12___ uwanja wa ndege. Kilichonifurahisha ni kule kutua kwa ndege na ___13___ angani kwa maringo. Ama kweli ___14___ wa ndege wana ___15___ kubwa mno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. kwanza | B. awali | C. mosi | D. twende |
| **12.** | A. ila | B. hadi | C. licha | D. kwenye |
| **13.** | A. kupanda | B. kuparaga | C. kutoboa | D. kupaa |
| **14.** | A. dereva | B. matwana | C. nahodha | D. rubani |
| **15.** | A. hukumu | B. jukumu | C. kiwango | D. ujuzi |

**Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo**

16. Ni orodha ipi yenye **viunganishi pekee**?
A. Safi , hodari, laini, dhaifu
B. Soma, cheza, jaza, imba
C. Aka! zii! ebo! shabash!
D. Wala, sembuse, kisha, bali

17. Sonara kwa pete, mgema kwa ___________.
A. ngoma B. tembo
C. pembe D. hema

18. **Kanusha sentensi:-**
Ungetembea ungefika
A. Hungetembea haungefika
B. Usingetembea usingefika
C. Usingetembea haungefika
D. Ungetembea usingefika

19. Kutokana na nomino *'zawadi'* tunapata kitenzi
A. zawadia B. zawadisha
C. kuzawadi D. zawidi

20. **Bainisha maneno yaliyopigiwa vistari katika sentensi ifuatayo:-**
Kamati ya bunge hilo ilijadili hoja nyingi na nyingine zikakosa wakati
A. kivumishi, kivumishi, kiwakilishi
B. kivumishi, kielezi, kiunganishi
C. kihusishi, kivumishi, kiwakilishi
D. kiwakilishi, kielezi, kuinganishi

21. **Toa udogo wa sentensi hii:-**
Mvulana mtundu aliumwa na mbwakoko viwili
A. Kijivulana kitundu kiliumwa na vijibwakoko viwili
B. Kivulana kitundu kiliumwa na vijibwakoko viwili
C. Kivulana kijitundu kiliumwa na vijibwavikoko viwili
D. Kivulana kitundu kiliumwa na vijiumbwakoko viwili

22. **Toa methali inayoafiki maelezo haya:-**
Mtu anayekabiliana na shida kisha akapata msaada japo kidogo bila shaka hawezi kukata tamaa. Atajitahidi shadidi na kujikakamua ili kuokoka au kufaulu.
A. Haba na haba hujaza kibaba
B. Kila mwanzo ni mzito
C. Msasi haogopi miba
D. Mbwa hafi maji akiona ufuko

23. Neno lipi si kisawe kati ya haya?
A. Jitimai B. Majonzi
C. Machozi D. Huzuni

24. Ni sentensi gani yenye *'na'* ya umilikaji?
A. Nyasi zimefyekwa na mkulima hodari
B. Nguo yangu na yako ndizo bora zaidi
C. Mchuuzi ana bidhaa nyingi sana
D. Wanaenda darasani kusoma

25. **Andika sentensi ifuatayo katika usemi taarifa:-**
"Nitaenda kesho kuogelea nikiwa na rafiki tangu" Juma alisema
A. Juma alisema ataenda kuogelea siku iliyofuatia akiwa na rafiki yake
B. Juma alisema angeenda kuogelea kesho akiwa na rafiki yake
C. Juma alisema ningeenda kuogelea siku iliyofuatia nikiwa na rafiki yake
D. Juma alisema angeenda kuogelea siku iliyofuata akiwa na rafiki yake

26. **Chagua kifungu sahihi:-**
Niliona _______ cha askari kikipiga kwata kandokando ya _______ la takataka.
A. kigaro/ jaa
B. kicha/lindi
C. kipeto/jaa
D. kigaro/pakacha

27. **Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:-**
Bata ametulia kwenye ua wa jirani
A. Bata wametulia kwenye maua ya jirani
B. Mabata yametulia kwenye maua ya majirani
C. Mabata wametulia kwenye nyua za majirani
D. Bata zimetulia kwenye nyua za jirani

28. Ikiwa Farida ni mtoto wa mwamu wangu, nitamwitaje?
A. Mpwa B. Binamu
C. Mkoi D. Mwanangu

29. Ni sentensi ipi iliyoakifishwa ipasavyo?
A. Ninapenda masomo yafuatayo, Kiswahili, dini na Hisabati
B. Kumbe mama yako ni daktari?
C. Mwanafunzi bora *(Bahati)* ametuzwa.
D. Sipendi kula wali, " mgeni alisema."

30. Chagua sentensi iliyo sahihi
A. Chupa zenye madawa zimevunjika
B. Chupa zenyewe zenye dawa zavunjika
C. Chupa enye dawa zimevunjika
D. Chupa zenye dawa zimevunjika

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31- 40.**

Nilibisha mlango wa ofisi ya mwalimu mkuu kwa shauku nyingi sana. Mchanganyiko wa hisia ulinipitia moyoni na mwili mzima. Huo ulikuwa muda ambao nilikuwa nimeusubiri sana kwa nia ya kujua nilichokivuna baada ya hekaheka za miaka minne ya kupanda na kupalilia masomo yangu.

Sikukutana na mwanafunzi yeyote nilipoingia shuleni wala sikumkuta yeyote nilipoingia ofisini mle. Mwalimu mkuu alikuwa ameketi mezani pake, huku akipapasapapasa ndevu zake kama ilivyo ada yake hasa awapo akiwaza.

"Shikamoo mwalimu" nilimsalimu. " Marahaba, hujambo?" akaitikia " sijambo mwalimu, habari za mwaka mpya?" nikaongezea. "Twashukuru Mungu, karibu kiti," akasema. " Asante sana mwalimu, " nikaitikia huku nikikalia kiti kilichokuwa kwenye upande wa pili wa meza.

Kwa muda wa dakika nzima hivi, mwalimu alinikazia macho pasi kuyapepesa. Nilihisi nikisisimkwa na malaika na kutiririkwa na kijasho chembamba. Nilitamani kuuliza ni nini kilikuwa cha mno bali ulimi **ulinigandia kinywani**. Nilihisi afueni si haba alipotazama kando na mara akaanza kupekuapekua karatasi zilizokuwa pale mezani.

Kimya kilitanda kwa dakika kadhaa. Sauti pekee iliyosikika ofisini mle ni ya saa iliyokuwa pale kiambazani. Kwa kukosa jingine la kufanya niliyageuza macho yangu kuitazama. Iliashiria saa mbili kamili asubuhi. Do! Hapo ndipo nilipowahi fursa ya kutanabahi kuwa nilikuwa nimetumia takribani dakika kumi tu kutoka nyumbani hadi shuleni. Sikuwa nimedhani kuwa nilikimbia kiasi kile.

"Moraa mwanangu!" sauti ya mwalimu ilinishtua na kunigutua. Sikuwa nimewahi kumsikia mwalimu mkuu akiniita ***'mwanangu'*** tena. Nilimzoea kuwa mkali daima asiyeweza kuita kwa njia hiyo yenye fadhili. Muda si muda akaendelea, "Nafurahi kuona una tamaa kubwa ya kujua matokeo yako ya mtihani wa kitaifa. Ni jambo zuri. Ulikuwa mwanafunzi hodari na bila shaka tulitazamia kuwa kama kawaida ungetutia fahari wakati wa matokeo. Hata hivyo, nasikitika kukufahamisha kuwa matokeo yako yamefutiliwa. Yalisemekana si halali"

Nilitamani ardhi ipasuke inimeze. Sikuwa nimewazia hilo. **Niliachama** bali neno hata moja halikunitoka. Mawazo yalinipitia kichwani kuhusu siku ile ya mtihani wa Kiswahili. Mimi na rafiki zangu Beti na Dora tulibadilishana kazi, tukazilinganisha, tukazifanyia marekebisho kabla ya kutabasamu. Tabasamu la ushindi, kumbe! Laiti tungalijua! Laiti ningalijua, nisingalikubaliana na rai ya Beti.

**31.** Msemaji anasema kuwa mchanganyiko wa hisia ulimpitia moyoni na mwilini mzima, unafikiri ni mchanganyiko wa hisia zipi?
A. Furaha na huzuni
B. Huzuni na wasiwasi
C. Furaha na wasiwasi
D. Furaha na nderemo

**32.** Ni muda upi ambao msemaji aliusubiri sana?
A. Wakati angepata fursa ya kuibisha ofisi ya mwalimu mkuu
B. Muda wa kupanda na kupalilia masomo yake
C, Muda wa kuukalia mtihani wake wa mwisho
D. Muda wa kupokea matokeo ya mtihani wake wa mwisho

**33.** Ni kawaida ya mwalimu mkuu kufanya nini akiwaza?
A. Kupapasapapasa ndevu zake
B. Kuketi mezani pake
C. Kukaa pekee yake ofisini
D. Kulipa ada yake

**34.** Mazungumzo baina ya Moraa na mwalimu mkuu yalianzaje?
A. Mwalimu alimkaribisha Moraa kitini
B. Moraa alimsabahi mwalimu
C. Moraa alimshukuru mwalimu
D. Mwalimu alimwamkua Moraa

**35.** Kwa nini mwalimu mkuu alinyamaza kwa dakika chache?
A. Alitaka kumkagua vizuri Moraa jinsi alivyokuwa
B. Hakujua aanzaje kumweleza Moraa yaliyokuwa yametokea
C. Alikuwa amejawa na hasira sana
D. Alimwogopa mno Moraa

**36.** ......... "Ulimi uligandia kinywani" ...... maana yake ni
A. niliyazuia maneno yangu
B. sikujua la kusema
C. maneno yalikosa kutoka
D. sikutaka kuzungumza

**37.** Kwa nini Moraa aligeuka kutazama saa iliyokuwa kiambazani?
A. Ajue mwalimu angepekua karatasi kwa dakika ngapi
B. Ajue alitumia muda gani kufika pale shuleni
C. Ahakikishe iwapo kweli alikimbia kwa kasi kama alivyofikiria
D. Ili kuupisha tu wakati akisubiri mwalimu azungumze

**38.** Kwa nini matokeo ya Moraa yalifutiliwa mbali?
A. Yalikuwa haramu
B. Hakuwa mwanafunzi hodari
C. Yalikuwa halali
D. Yalikuwa ya kuonea fahari mno

**39.** Kulingana na aya ya mwisho, baada ya kupata habari kuhusu matokeo yake, Moraa:
A. alitabasamu kwa sababu ya ushidi wake
B. alisherehekea pamoja na marafiki wake Beti na Dora
C. alishtuka mno na kujutia matendo yake
D. alipinga kabisi rai ya rafikiye Beti

**40.** Si kweli kwamba Moraa, Beti na Dora walikuwa wanafunzi
A. hodari
B. waaminifu
C. marafiki
D. watahiniwa

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41- 50.**

Dawa za kulevya ni dondandugu - suala nyeti linalofaa kupewa kipaumbele leo kesho. Mwongo mmoja uliopita dawa hizi za kulevya hazikuwa tishio kubwa zaidi. Sasa ni jinamizi, mambo yamechacha hadi yakachacharika. Mihadarati kweli imevuruga wazee kwa vijana, wenye vyeo na akina yakhe. Iwapo hujaathirika upo uwezekano umehasiriwa kwa njia moja au nyingine. Je, ni nani atavumbua makombora ya kuangamiza dawa hizi?

Uraibu wa mihadarati huzua maradhi sugu. Kwa mfano, pombe hudhuru maini, sigara nayo huleta kansa au saratani ya mapafu. Aidha, bangi huathiri akili ya mtumiaji, ukiitumia kwa muda ayami, husababisha wazimu.

Isitoshe, watumwa wawa hawa wa mihadarati aghalabu hawawi na adabu na nidhamu. Haya zao huwatupia mbwakoko eti. Hutema matusi kiholela bila kujali umri wala cheo cha msikilizaji. Wengi vile vile wahusishwa na visa vya kuachamisha vinywa. Hushindwa kudhibiti hisia zao. Si **ibura** kulipata jibaba la mtu likibeua hadharani au kukimbizana na vidosho vichanga mitaani.

Dawa hizi haramu huwafanya wengi kusahau majukumu yao ya kimsingi. Hela nyingi huishia kwa dawa hizi zilizo ghali. Nao walanguzi huzidisha juhudi zao za kupanua biashara hata katika taasisi za elimu. Utawaona watoto warembo wametelekezwa kiasi cha kuanza uchokora mitaani ilhali wazazi wao wapo. Je, huu ni ungwana?

Hakika, watumwa hawa hunaswa na minyororo mizito ya upofu. Hugeuka kuwa kiduko asiyeonywa hata ajiingizapo katika anasa. Raha za dunia nazo humzalia matunda ya maradhi kama vile ukimwi na mengineyo ya zinaa. Familia huvunjika baada ya wazazi kutalakiana. Watoto huzidishiwa fadhila wakiachwa kuyumba kama makinda waliofukuzwa viotani.

Kwa hakika, **mihadarati ni asali sumu** ituangamizayo bila fahamu zetu. Ni baa kubwa linalifaa kung'olewa kabisa na mizizi yake iliyoenea kama magugu ya kifauongo shambani.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza
A. miaka kumi iliyopita athari za dawa za kulevya hazikuwa zimeenea sana
B. vijana wamesumbuliwa na mihadarati zaidi ya kundi lolote lile la watu
C. makombora ndiyo yatakayotumiwa kumaliza maangamizi ya mihadarati
D. dawa za kulevya zimehalalishawa kikatiba

**42.** Watumwa wa mihadarati
A. hukosa haya ya kufanya maovu na kuwa wazimu
B. mara nyingi hupotoka kimaadili
C. kuwauzia hasa matajiri dawa hizi
D. wamefungwa jela na hawana uhuru

**43.** Aya ya tatu imeonyesha kuwa
A. maradhi ya zinaa kama vile ukimwi husababishwa aghalabu na uraibu wa dawa za kulevya
B. watoto wametekelezewa matakwa yao vilivyo
C. walevi wa mihadarati hubeua hadharani kwa muhali sana
D. mmomonyoko wa maadili umesababishwa na dawa hizi haramu

**44.** Kulingana na kifungu
A. mihadarati hufaidi kwa kiasi kidogo sana
B. anasa huathiri wazee zaidi kiliko vijana
C. usuhuba wa kimapenzi kati ya wasichana wadogo na wanaume hukuzwa na taasisi za elimu
D. athari za dawa za kulevya zimelemaza maendeleo kwani wengi wamehasiriwa na kuathiriwa

**45.** Ni ipi si dawa ya kulevya?
A. Sharubati
B. Mirungi
C. Hashishi
D. Sigara

**46.** Mwandishi amedhihirisha
A. walanguzi wa dawa hizi ni wanafunzi
B. mihadarati ni asali iliyo na sumu
C. saula la mihadarati ni changamoto nchini
D. tamaa ya kutaka kujiinua kiuchumi kwa njia mbadala hufaidi

**47.** **"Mihadarati ni asali sumu...."** Hii ni fani gani ya lugha?
A. Methali
B. Istiara
C. Nahau
D. Tashbihi

**48.** Ni wazi kwamba kumaliza donda ndugu la mihadarati
A. walanguzi wote wa dawa hizi watiwe mbaroni
B. vijana wasipewe uhuru wa kutangamana
C. tunafaa kung'oa mizizi ya kifauongo mashambani
D. ni vizuri kuondoa kiini cha usambazaji na uraibu wa mihadarati

**49.** Chagua neno ***baki*** katika kundi hili
A. chirwa
B. ukimwi
C. kisalisali
D. sekeneko

**50.** Chagua mada kuu ya kifungu hiki
A. Uozo katika jamii
B. Uraibu wa dawa za kulevya
C. Mihadarati na athari zake
D. Dawa za kulevya ni kitega uchumi